

Vital Records Office
P.O. Box 70
Burlington, VT 05402

Jinsi ya Kutuma Ombi la Cheti cha Kuzaliwa Kilichochelewa Kuandikishwa

Fomu zilizoambatishwa za **Ombi la Cheti cha Kuzaliwa Kilichochelewa Kuandikishwa na Taarifa Itakayoandikwa kwenye Cheti cha Kuzaliwa Kilichochelewa Kuandikishwa** hutumiwa kuandikisha mtoto aliyezaliwa katika jimbo la Vermont na kuzaliwa kwake hakukuandikishwa katika mji alipozaliwa.

Maagizo ya kutuma ombi la cheti cha kuzaliwa kilichochelewa kuandikishwa:

1. Jaza Ombi la Cheti cha Kuzaliwa Kilichochelewa Kuandikishwa na Taarifa Itakayoandikwa kwenye Cheti cha Kuzaliwa Kilichochelewa Kuandikishwa.
2. Peleka fomu kwa mthibitishaji wa umma na uandike jina lako la sasa la kisheria mbele ya mthibitishaji wa umma.
3. Kusanya hati za awali au zilizoidhinishwa zinazothibitisha umri, mahali pa kuzaliwa na taarifa ya wazazi:

Kwa mtu mwenye umri wa miaka 10 au zaidi, hati tatu zilizothibitishwa au za awali zinahitajika ili kuunga mkono madai ya ombi la cheti kilichochelewa kuandikishwa huko Vermont. Kila hati lazima ionyeshe tarehe ya kuzaliwa au umri wa mtu huyo na lazima iwe iliandikwa angalau miaka 10 kabla ya tarehe ya ombi la cheti kilichochelewa kuandikishwa, au ndani ya miaka 3 baada ya tarehe ya kuzaliwa. Angalau hati moja lazima ionyeshe kuwa mtu huyo alizaliwa katika jimbo la Vermont na hati moja lazima iwe na jina la angalau mzazi mmoja. Rejelea orodha ya hati za msingi kwenye ukurasa unaofuata. *Hati zinaweza kuchunguzwa na kuidhinishwa na Msajili wa Jimbo.*

Kwa mtu mwenye umri wa chini ya miaka 10, hati mbili zilizothibitishwa au za awali zinahitajika ili kuunga mkono madai ya ombi la cheti kilichochelewa kuandikishwa huko Vermont. Hati ya kwanza lazima ionyeshe kwamba mama alikuwa Vermont alipojifungua. Hati ya pili lazima ionyeshe jina la mtoto, tarehe ya kuzaliwa, kuwa mtu huyo alizaliwa katika jimbo la Vermont na jina la angalau mzazi mmoja. Rejelea orodha ya hati za msingi kwenye ukurasa unaofuata. *Hati zinaweza kuchunguzwa na kuidhinishwa na Msajili wa Jimbo.*

4. Wasilisha fomu na hati zifuatazo zinazounga mkono madai yako:
 - Ombi la Cheti cha Kuzaliwa Kilichochelewa Kuandikishwa lililojazwa na kuthibitishwa
 - Taarifa Itakayoandikwa kwenye Cheti cha Kuzaliwa Kilichochelewa Kuandikishwa iliojazwa na kuthibitishwa
 - hati asili au zilizoidhinishwa zinazounga mkono madai yako, zinazothibitisha umri, mahali pa kuzaliwa na taarifa ya wazazi

Kwa: Vermont Department of Health - Vital Records Office
108 Cherry Street, PO Box 70
Burlington, VT 05402

Mwombaji atarejeshewa hati zote asili na nakala za hati zilizoidhinishwa. Nakala ambazo hazijaidhinishwa hazitakubaliwa.

Hati za Msingi za kuthibitisha ukweli wa cheti cha kuzaliwa kilichochelewa kuandikishwa:

- Kumbukumbu au waraka wa kuzaliwa wa hospitali
- Kumbukumbu au waraka wa kuzaliwa wa ofisi ya daktari
- Kumbukumbu au waraka wa kuzaliwa wa mkunga
- Kumbukumbu ya Hesabu ya Sensa ya Marekani
- Maombi ya leseni ya ndoa
- Maombi ya akaunti ya Usalama wa Kijamii
- Kumbukumbu ya kuwa jeshini (sio cheti)
- Pasipoti
- Sensa ya shule au rekodi ya kuandikishwa shulenii
- Hati ya bima ya maisha – hati kamili ya bima inayoonyesha nambari ya bima na tarehe ilipotolewa.
- Rekodi za ajira
- Rekodi ya matibabu, hospitali au matibabu ya meno
- Ushahidi mwingine ulioombwa na Msajili wa Jimbo

Kumbuka: Hati za kiapo za kibinafsi haziwezi kuwasilishwa kama Hati za Msingi.

Kwa nini Uthibitisho Unahitajika ili uandikishe Cheti cha Kuzaliwa Kilichochelewa Kuandikishwa?

Cheti cha kuzaliwa ni hati muhimu inayothibitisha uraia wa Marekani na umri. Cheti cha Kuzaliwa Kilichochelewa Kuandikishwa kina thamani sawa na hati zinazotumiwa kuthibitisha ukweli kuhusu kuzaliwa kwa mtu. Hii ndio maana hati mahususi zinazounga mkono ombi lako zinahitajika. Hati hizo lazima ziwe asili au zilizothibitishwa na zisibadilishwe, ili cheti chako cha kuzaliwa kilichochelewa kuandikishwa kiwe sahihi.

Je, una maswali?

Pigia simu Ofisi ya Rekodi Muhimu yaani Vital Records - Vermont Department of Health ukiwa na maswali yoyote kuhusu vyeti vya kuzaliwa vilivyochelewa kuandikishwa. Unaweza kuwasiliana na Msimamizi wa Vital Records kwa (802) 863-7278.